



JAMHURI YA KENYA

WIZARA YA MAZINGIRA, MABADILIKO TABIA NCHI NA MISITU

IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA

Dagoretti Corner, Ngong Road, SLP 30259, 00100 GPO, Nairobi, Kenya

Simu: 254 (0) 20 3867880-7, 0724 255 153/4

Barua pepe: [director@meteo.go.ke](mailto:director@meteo.go.ke), [info@meteo.go.ke](mailto:info@meteo.go.ke)

X: [@MeteoKenya](https://twitter.com/MeteoKenya)

## 1. UTABIRI WA HALI YA HEWA KWA MSIMU WA MASIKA: MACHI – MEI 2025

### 1.1 Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Masika kipindi cha Machi – Mei, 2025

Tathmini ya hali ya hewa msimu huu wa mvua za masika inaonyesha kwamba, viwango vya mvua ambavyo vinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi vinakadiliwa kuwa vya chini, hasa katika kanda za Mashariki ya Kenya na kaskazini ya mwambao wa Pwani. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya Magharibi mwa nchi na nyanda za chini za mashariki ya Kenya yanatarajiwa kuwa na mvua ya kiwango cha zaidi ya kawaida. Vilevile, kanda za juu ya kaskazini na katikati mwa bonde la ufa, nyanda za mashariki mwa bonde la ufa, Kusini na katikati ya pwani, kiwango cha mvua kinatarajiwa kuwa cha kawaida mpaka chini ya kawaida. Mgao wa mvua hizi unaonyesha kwamba, sehemu nyingi kwenye kanda za mashariki mwa nchi zinatarajiwa kuwa kavu kwenye mwezi wa Machi. Mgao huu unatarajiwa kuwa kileleni katika maeneo mengi nchini kwenye mwezi wa Aprili ila maeneo ya pwani kilele chake kinatarajiwa Mei, japo kiwango chake kitakuwa cha chini. Zaidi ya hayo, maeneo mengine nchini yana uwezekano mkubwa wa kupata mvua za dhoruba za mara kwa mara. Hali hii itakuwa imechochewa na hali ya joto (SSTS) kwenye bahari ya hindi, pasifiki na atlantiki na pia ushawishi wa mambo ya kijografia, na viashiria muonekano vinavyoathiri mwelekeo wa hali ya hewa nchini.

Kwa upande mwingine, utabiri wa joto unaonyesha kwamba eneo kubwa nchini msimu huu, linatarajiwa kuwa na hali ya joto ya juu kuzidi wastani lakini viwango vyake vinatofautiana kwa maeneo tofauti nchini. Kwa kuangazia maeneo ya kaskazini ya nchi na baadhi ya sehemu za kusini zinatarajia hali ya joto kufikia nyusi za juu zaidi ya maeneo mengine nchini.

### 1.2 Utabiri wa kina katika Msimu wa Masika (Machi-Mei) 2025 ni kama ifuatavyo: Ziwa Viktoria, Nyanda za juu magharibi ya Bonde la Ufa na Kaunti za Katikati na Kusini ya Bonde la Ufa:

{{Siaya, Kisumu, Homa Bay, Migori, Kisii, Nyamira, Uasin Gishu, kusini magharibi ya West Pokot, baadhi ya maeneo ya Elgeyo Marakwet, Nandi, Kericho, Bungoma, Kakamega, Busia, Trans Nzoia, Vihiga, Magharibi ya Nakuru, baadhi ya maeneo ya Narok) baadhi ya maeneo kaskazini magharibi mwa Turkana}. Mvua katika kaunti hizi inatarajiwa kuendelea kwenye msimu. Kiwango cha mvua kinatarajiwa kuwa cha kukaribia au kupita kiwango cha wastani.

**Kaunti za Kaskazini Magharibi:** (Samburu na baadhi ya maeneo ya Turkana). Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea mvua za kiwango cha karibu na wastani mpaka kile cha chini ya wastani. Mgao wa mvua hizi unatarajiwa kuwa wa duni kwa muda na kuenea kwake.

**Kaunti za nyanda za juu mashariki ya Bonde la Ufa:** {(Pamoja na maeneo ya Nairobi) (Nyandarua, Nyeri, Kirinyaga, Murang'a, Kiambu, Meru, Embu, Tharaka Nithi, Laikipia na Nairobi), baadhi ya maeneo ya Nakuru, baadhi ya maeneo ya Isiolo}. Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea mvua za kiwango cha karibu na wastani mpaka kile cha chini ya wastani. Mgao wa mvua hizi unatarajiwa kuwa wa kuridhisha kwa muda na kuenea kwake.

**Kaunti za Kusini-Mashariki ya Kenya:** (Kitui, Makueni, Machakos, mashariki ya Taita Taveta, na Kusini-Mashariki ya Kajiado). Maeneo haya yanatarajiwa kupokea kiwango cha mvua ya wastani mpaka chini ya wastani. Mgao wa mvua hizi unatarajiwa kuwa wa duni.

**Kaunti za Kaskazini Mashariki:** {(Mandera, Wajir, Garissa, baadhi ya sehemu za Isiolo, Marsabit,) na maeneo ya Lamu}. Maeneo haya yanatarajiwa kupokea mvua za mara kwa mara na kiwango chake kinatazamiwa kuwa cha chini ya kawaida. Mgao wake unatarajiwa kuwa wa kutoridhisha kwa muda na kuenea kwake.

**Ukanda wa Pwani:** (Mombasa, Kwale na Kaunti za Kilifi). Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea mvua za kiwango cha wastani mpaka chini ya wastani. Vilevile, eneo hili lina uwezekano wa kukumbwa na vipindi vya ukavu vya mara kwa mara. Usambazaji wa mvua unatarajiwa kuwa duni kwa muda na kuenea kwake.

## **2. TAARIFA YA TAREHE ZA MWANZO, KIKOMO NA MGAO WA MVUA ZA MASIKA 2025**

Utabiri wa tarehe za mwanzo, kikomo mgao wa mvua za masika umetokana na uchambuzi wa tarakimu za miaka iliyopita ambayo ilikuwa na dhalili sawia na za mwaka huu.

### **2.1 TAREHE ZA MIANZO NA KIKOMO CHA MVUA ZA MASIKA 2025**

Tarehe za mianzo na kikomo kwa mvua za masika katika Kaunti mbali mbali ni kama ifuatavyo:

**Nyanda za kusini mwa bonde la ufa, Ziwa Victoria, na sehemu nyingi za nyanda za Magharibi ya Bonde la Ufa:** (Homa Bay, Migori, Kisumu, Busia, Siaya, Narok, Bomet, Kisii, Nyamira, Kericho, Nandi, Kakamega, Vihiga). Mvua inaendelea kutoka Februari na itakumbwa na vipindi vya ukavu vya mara kwa mara. Kikomo chake kinatarajiwa kuwa Juni. Mgao wake unatarajiwa kuwa mzuri.

**Kaunti za Kati na Kaskazini ya Bonde la Ufa na baadhi ya maeneo ya Magharibi ya Bonde la Ufa:** (Nakuru, Baringo, Sehemu za Magharibi ya Laikipia, Elgeyo Marakwet, Uasin Gishu, Trans-Nzoia, Bungoma na Sehemu za Kusini za West Pokot). Mvua inatarajiwa mwezi wa Februari ikifuatiwa na vipindi vya ukavu kwenye wiki ya nne ya Machi hadi ya kwanza ya Aprili. Kikomo chake kinatarajiwa kuwa Juni. Mgao wake ni wa kuridhisha.

**Kaunti zilizo nyanda za juu mashariki ya Bonde la Ufa Pamoja na Nairobi:** (Nyandarua, Nyeri, Kirinyaga, Murang'a, Kiambu, Tharaka nithi, Meru, Embu, Nairobi na mashariki ya Laikipia). Mvua za mara kwa mara zinatarajiwa mwezi wa Februari, ikifuatiwa na kipindi cha ukavu. Mwanzo wa mvua unatarajiwa katika wiki ya nne ya Machi hadi wiki ya kwanza ya Aprili. Kikomo chake kinatarajiwa kuwa kati ya wiki ya tatu hadi ya nne ya Mei. Usambazaji wa mvua unatarajiwa kuwa mzuri.

**Kaunti za Kusini-Mashariki:** (Kajiado, Kitui, Makueni, Machakos, Tana River na Taita Taveta). Mvua ya mara kwa mara inatarajiwa kwenye mwezi wa Februari, ikifuatiwa na kipindi cha ukavu. Mwanzo wa mvua hizi unatarajiwa kati ya wiki ya nne ya Machi hadi wiki ya kwanza ya Aprili. Kikomo chake kinakadiriwa kuwa kati ya wiki ya tatu hadi ya nne ya Mei. Usambazaji wa mvua unatarajiwa kuwa wa wastani hadi duni.

**Eneo la Kaskazini ya Pwani:** (Lamu, Sehemu za Pwani za Tana River, na Sehemu za Kaskazini mwa Kilifi). Mvua inatarajiwa kati ya wiki ya pili hadi ya tatu ya Aprili. Mvua hii itaendelea hadi Juni. Ugawaji wake unatarajiwa kuwa duni.

**Eneo la Kusini ya Pwani:** (Mombasa, Kwale na Sehemu za Kilifi Kusini). Mvua inatarajiwa kuanzia wiki ya nne ya Machi hadi wiki ya kwanza ya Aprili, inakadiriwa kuendelea hadi Juni. Mgao wake unatarajiwa kuwa kuridhisha hadi duni.

**Kaskazini Magharibi** (Turkana, Samburu na Kaskazini ya West Pokot): Mvua ya mara kwa mara inatarajiwa mwezi wa Machi. Kuanza kwa mvua hii kunatarajiwa kwenye wiki ya kwanza hadi ya pili ya Aprili. Mgao wa mvua unatarajiwa kuwa duni.

**Kaskazini mashariki** (Marsabit, Mandera, Wajir, Isiolo, Garissa): Kuanza kwa mvua hii kunatarajiwa kwenye wiki ya kwanza hadi ya pili ya Aprili. Mgao wa mvua unatarajiwa kuwa duni.

#### **4. Athari zinazotarajiwa kutokana na Mvua za Masika 2025**

Mvua za kiwango cha wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi nchini katika msimu huu wa masika 2025. Mvua hizi zinatarajiwa kuleta athari mbalimbali na hasa katika sekta zote nchini. Athari kuu ambazo huenda zikajitokeza zimejadiliwa na kuafikiwa na wadau na wataalamu wa sekta husika.

***Kumbuka: Utabiri huu wa mvua za masika unafaa utumike pamoja na tabiri za hali ya hewa za siku 5, tabiri za wiki, tabiri za mwezi zikifuatanishwa na jumbe fupi boresha, ripoti za ushauri na jumbe za athari Pamoja na tabiri za wiki na mwezi za Kaunti tokea Ofisi za huduma ya hali ya hewa katika kila Kaunti nchini.***



Dr. David Gikungu

**MKURUGENZI WA IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA NCHINI KENYA**

